MAJIBU YENYE FAIDA NO.2

KUHUSU

MASWALI YANAYOFUNGAMANA NA MIFUMO MIPYA

MTUNZI: SHEIKH SWALEH BIN FAWZAN BIN ABDILLAH AL FAWZAN

MFASIRI: ABUL AALIYAH UMAR BIN MUHAMMAD BIN KONDO

PONGWE – TANGA – TANZANIA

SWALI LA PILI:

Vituo vya majira ya joto (summer centers) (المَرَاكِز الصَيفِيَة) hufanywa humo Tamthilia (maigizo) na nyimbo, basi ni ipi rai yenu katika hilo?

JIBU : Ni wajibu kwa wasimamizi wa vituo vya majira ya joto wazuie vitu ambavyo havina faida yoyote humo,au vina madhara kwa wanafunzi,na wawafundishe Qur'an na Sunna,Hadithi,Fiqhi,na Lugha ya kiarabu,na katika haya kuna kutosheka na waka na kushughulika na wakati na kujiepusha na vitu vingine.

Hali kadhalika kuwafundisha Elimu ambazo wanazihitajia katika Dunia yao: kama kuandika,Hesabu,na Ustadi mzuri (Useful skills).

Ama vile vitu wanavyoviita Burudani hivi kiuahalisia havitakikani kuepo katika program (zote) kwa sababu hakika vitu hivyo vinakata sehemu katika wakati bila ya faida yoyote

bali huwenda vikawashughulisha na vikawasahaulisha faida ambayo wameijia kwa ajili yake.

Na miongoni mwa hivyo:

Tamthilia (Maigizo) na Nyimbo[1] hakika hali ilivyo hivyo ni pumbazo na mchezo tu vinawazoesha wanafunzi kufuatilia Maigizo na miziki ambayo inasambazwa kupitia vyombo mbalimbali vya matangazo.

---

[1] - Na kuziita hizi nyimbo "nyimbo za kiislamu"(ANAASHIID ISLAAMIYYAH) ni makosa,kwa sababu uislamu haukuwekea sharia ya nyimbo bali hakika sivingine uislamu umetuekea kumdhukuru Allah,kusoma Qur'an na kujifundisha Elimu yenye manufaa.Ama Anaasheed (nyimbo) ni Dini ya Masufi watu wa bidaa ambao wameifanya Dini yao pumbazo na mchezo na kuzigeuza nyimbo ni katika Dini huku ni kujifananisha na Manasara (wakiristo).